GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXXIV Nam. 7405 **10 Oktoba 2025** **Bei Shs.5,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO **UK**

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam 2 ya 2005
Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa misingi ya Sharia)..... 1227

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Sheria lilotajwa hapo chini imetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Sheria

Nam. 90:-Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa misingi ya Sharia)

TANGAZO NAM. 90

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (SKIMU YA HIFADHI YA JAMII KWA MISINGI YA SHARIA)

[Chini ya kifungu cha 44(2)]

MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI **MAELEZO**

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA SKIMU YA HIFADHI YA JAMII KWA MISINGI YA SHARIA

4. Uanzishwaji wa Skimu.
5. Fedha za Skimu.
6. Malengo ya Skimu.
7. Kazi za Skimu.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA SKIMU

8. Kamati ya Ushauri wa Sharia.
9. Kazi za Kamati ya Ushauri wa Sharia.

SEHEMU YA NNE
USAJILI WA WANACHAMA

10. Usajili wa wanachama.
11. Usajili wa wanachama wa kikundi au jumuiya.
12. Kitambulisho cha Uanachama.

SEHEMU YA TANO
MICHANGO NA TARATIBU ZA UWASILISHAJI WA MICHANGO

13. Wajibu wa kuchangia katika Skimu.
14. Utaratibu na njia za kuwasilisha michango.
15. Uwasilishaji wa michango kwa wanachama wa kikundi.
16. Mikataba ya upokeaji wa michango.
17. Utoaji wa taarifa za hesabu za mwanachama.

SEHEMU YA SITA
MAFAO, SIFA NA UTARATIBU WA MALIPO WA MAFAO

18. Mafao yatakayolipwa na Skimu.
19. Sifa za kulipwa fao la uzeeni.
20. Sifa za kulipwa fao la ulemavu.
21. Sifa za kulipwa fao la urithi.
22. Sifa za kulipwa fao la uzazi.
23. Sifa za kulipwa fao la upotevu wa ajira.
24. Sifa za kulipwa fao la kuumia kazini.
25. Ukokotoaji wa mafao.
26. Utaratibu wa kuomba mafao.
27. Kutostahili kupata mafao zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

SEHEMU YA SABA
UWEKEZAJI WA SKIMU

28. Taratibu za uwekezaji.
29. Maeneo ya uwekezaji.
30. Mikataba itakayotumiwa na Skimu katika uwekezaji.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA FEDHA

31. Matumizi ya Fedha za Skimu.
32. Hesabu za Skimu.
33. Bajeti ya Skimu.
34. Ripoti za mwaka za Skimu.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI MENGINEYO

35. Michango kuwa katika dhamana ya Skimu.
36. Tathmini ya uhimilivu wa Skimu.
37. Makubaliano mbadala.

JADWELI

TANGAZO NAM. 90

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (SKIMU YA HIFADHI YA JAMII KWA MISINGI YA SHARIA), 2025
[Chini ya kifungu cha 44(2)]

KWA UWEZO niliopewa chini ya kifungu cha 44(2) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005, **Mimi, DKT. SAADA MKUYA SALUM**, Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango natunga Kanuni zifuatazo:

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Sharia), 2025 na zitaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Matumizi.

2. Kanuni hizi zitatumika katika uendeshaji na usimamizi wa Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Sharia.

Ufafanuzi.

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria;

"Fatwa" maana yake ni uamuzi na hukumu zinazoendana na misingi ya sharia;

"mkataba wa ukodishaji" maana yake ni mkataba ambapo upande mmoja unahamisha haki ya matumizi ya kitu kwa upande mwengine kwa muda maalumu na kwa makubaliano ya malipo maalumu bila ya kuhamisha umiliki wa kitu husika;

"mkataba wa kuuziana" maana yake ni mkataba wa mauziano ya muda mrefu baina ya muuzaji na mnunuzi unaohusisha kujenga au kutengeneza kitu kinachotarajiwa kukamilika baada ya muda maalumu na kwa kufanya malipo yaliyokubaliwa baina ya pande mbili ambayo yatalipwa mwanzoni au kabla ya mradi kukamilika;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Ushauri wa Sharia iliyoanzishwa chini ya kanuni ya 8(1) ya Kanuni hizi;

"michango" maana yake ni fedha zinazochangiwa na mwanachama au mwajiri wa mwanachama katika Skimu kwa ajili ya uwekezaji, akiba, sadaka au vyenginevyo;

"mafao" maana yake ni mafao yanayolipwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Mkurugenzi Mwendeshaji" maana yake ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar uliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria;

"mkataba wa ushirika" maana yake ni mkataba wa mashirikiano ya kiuwekezaji ambapo washiriki hutoa mali au fedha kwa kiwango walichokubaliana na kisha kugawana faida na hasara kwa mujibu wa mchango wa kila mmoja;

"salam" maana yake ni mkataba wa mauziano ya muda mrefu baina ya muuzaji na mnunuzi unaohusisha kitu kinachotarajiwa kukamilika baada ya muda maalumu na kwa kufanya malipo yaliyokubaliwa baina ya pande mbili ambayo yatalipwa mwanzoni au kabla ya mradi kukamilika;

"Sharia" maana yake ni Sheria za Kiislamu ikijumuisha Quran, Hadith, Makubaliano ya Maulamaa na vyanzo vyengine vya Sharia za Kiislamu;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005;

"Skimu" maana yake ni Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Sharia iliyoanzishwa chini ya masharti ya kanuni ya 4 ya Kanuni hizi;

"mkataba ya uwakala wa uwekezaji" maana yake ni aina ya mkataba wa uwakala ambapo pande mbili zinakubaliana kwa lengo la uwekezaji;

"wategemezi" maana yake ni warithi halali wa mwanachama marehemu; na

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya fedha.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA SKIMU YA HIFADHI YA JAMII KWA MISINGI YA SHARIA

Uanzishwaji wa Skimu.

4.-(1) Kunaanzishwa Skimu ambayo itajulikana kama Skimu ya Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Sharia kwa ufupisho wake ni ZSSF SHARIA SCHEME.

(2) Skimu itafanya kazi katika mifumo miwili ambayo ni:

(a) mfumo wa lazima kwa wafanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi watakaochagua kujiunga kwa mara ya kwanza katika Skimu au wanachama wa Mfuko watakaohamia katika Skimu kutoka Mfuko Mkuu baada ya kuanzishwa kwa Skimu hii; na

(b) mfumo wa hiari kwa watu binafsi watakaojiunga na Skimu.

Fedha za Skimu.

5. Vyanzo vya fedha vya Skimu ni:

(a) michango itakayolipwa na wanachama au waajiri kama ilivyoainishwa katika Sheria;

(b) mapato yatokanayo na uwekezaji wa fedha za Skimu; na

(c) fedha yoyote itakayopatikana kihalali na Skimu.

Malengo ya Skimu.

6. Malengo ya Skimu yatakuwa ni:

(a) kutoa hifadhi ya jamii kwa kufuata misingi ya Sharia;

(b) kufanya uwekezaji wa fedha za Skimu kwa kufuata misingi ya Sharia;

(c) kuhakikisha kuwa wanachama wanalindwa dhidi ya majanga ya kiuchumi na kijamii yanayotokana na matukio yasiyotabirika ikiwemo uzee, ajali, kifo, maradhi na kupoteza ajira kwa kufuata misingi ya Sharia; na

(d) kutekeleza Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar katika maeneo ambayo Skimu inahusika kwa kufuata misingi ya Sharia.

Kazi za Skimu.

7. Skimu itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusajili wanachama;

(b) kupokea na kukusanya michango ya wanachama;

(c) kulipa mafao ya hifadhi ya jamii kwa kufuata misingi ya Sharia;

(d) kuwekeza fedha zinazokusanywa katika miradi na yenye kuzingatia na kufuata misingi ya Sharia;

(e) kuweka na kutunza kumbukumbu za wanachama na michango itakayolipwa;

(f) kutoa elimu inayohusiana na umuhimu wa hifadhi ya jamii kwa misingi ya Sharia;

(g) kutoa taarifa za maendeleo ya Skimu kwa wanachama na wadau wengine;

(h) kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kuimarisha utoaji hifadhi ya jamii kwa misingi ya Sharia;

(i) kutayarisha na kuwasilisha ripoti za robo mwaka na ripoti za mwaka kwa Bodi;

(j) kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kuibua, kubuni na kuanzisha mafao, bidhaa au huduma mpya;

(k) kushirikiana na wadau au taasisi nyengine katika kutanua wigo wa utoaji wa hifadhi ya jamii kwa misingi ya sharia; na

(l) kufanya kazi nyengine yoyote ambayo itakuwa muhimu katika kuimarisha na kufanikisha malengo ya Skimu.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI WA SKIMU

Kamati ya Ushauri wa Sharia.

8.-(1) Kunaanzishwa Kamati ya Ushauri wa Sharia ambayo itaundwa na wajumbe watano ambao watateuliwa na Mwenyekiti wa Bodi.

(2) Mwenyekiti wa Kamati atateuliwa miongoni wa wajumbe wa Kamati.

(3) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Ushauri ya Sharia ikiwa mtu huyo, ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sharia, mfumo wa fedha wa kiislamu au fani nyengine zinazofanana na hizo kutoka katika taasisi inyotambuliwa na Serikali;na

(b) uzoefu wa kazi katika Kamati au Bodi ya Sharia, kufundisha au kufanya utafiti katika kazi zinazofanana na hizi.

Kazi za Kamati ya Ushauri wa Sharia.

9. Kamati ya Ushauri wa Sharia itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutoa ushauri juu ya uendeshaji wa Skimu kwa Bodi;

(b) kutoa fatwa kuhusiana na masuala ya kisharia yanayohusiana na Skimu;

(c) kutoa ushauri juu ya sera, miongozo na kanuni za uendeshaji wa Skimu kwa Bodi;

(d) kutoa ushauri juu ya huduma na mafao yanayotolewa na Skimu chini ya Kanuni hizi kwa kufuata misingi ya Sharia;

(e) kuhakikisha kuwa uwekezaji utakaofanywa na Skimu unafanyika kwa kufuata misingi ya Sharia;

(f) kutoa mapendekezo juu ya mambo mbalimbali yanayohusiana na Sharia yatakayowasilishwa katika Kamati;

(g) kuwasilisha mapendekezo ya Kamati kwa Bodi juu ya mambo mbalimbali yanayowasilishwa kwa ajili ya kuidhinishwa; na

(h) kufanya kazi nyengine yoyote kama Bodi itakavyoona inafaa.

SEHEMU YA NNE
USAJILI WA WANACHAMA

Usajili wa wanachama.

10.-(1) Mtu yeyote anayekusudiwa kusajiliwa kuwa mwanachama katika Skimu atawasilisha maombi kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kwa kujaza Fomu Nambari ISS1 kama ilivyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kusajiliwa kuwa mwanachama katika Skimu endapo mtu huyo:

(a) ni mtanzania au Diaspora;

(b) ana umri wa kuanzia miaka kumi na nane; na

(c) ana ajira, kazi au shughuli ya kiuchumi inayompatia kipato cha halali.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, mtu yeyote ambaye ni mwanachama wa Mfuko, kabla ya kuanzishwa Skimu, anaweza kuhama na kuhamisha michango yake kutoka Mfuko Mkuu na kujiunga na Skimu kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika miongozo.

(4) Mwanachama ambaye atajiunga na Mfuko baada ya kuanzishwa kwa Skimu hii atakuwa na fursa ya kuchagua kujiunga moja kwa moja katika Skimu au kujiunga katika Mfuko Mkuu.

(5) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (4) ya kanuni hii, mtu yeyote hatozuiliwa kuwa mwanachama wa Mfuko na kuwa mwanachama katika Skimu kwa hiari kwa wakati mmoja.

(6) Maombi chini ya masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii yataambatanishwa na:

(a) picha ya pasipoti iliyopigwa karibuni;

(b) nakala ya cheti cha kuzaliwa;

(c) nakala ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi au Kitambulisho cha Taifa; na

(d) nyaraka nyengine yoyote ambayo Mkurugenzi Mwendeshaji ataona ni muhimu katika kukamilisha usajili wa mwanachama husika.

Usajili wa wanachama wa kikundi au jumuiya.

11.-(1) Watu waliojikusanya kama kikundi au jumuiya inayofanya kazi au shughuli maalumu ya kiuchumi au ya kujipatia kipato wanaweza kusajiliwa kuwa wanachama katika Skimu kama kikundi au jumuiya kwa kujaza Fomu ya Maombi ya Usajili wa Kikundi au Jumuiya kama ilivyoainisha katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(2) Watu watakaosajiliwa kama kikundi au jumuiya watawasilisha nyaraka zifuatazo:

(a) hati ya usajili wa kikundi au jumuiya kutoka mamlaka husika iwapo kikundi au jumuiya imesajiliwa;

(b) orodha halisi ya wanakikundi au jumuiya ambao wanaomba kusajiliwa pamoja na picha zao ya aina ya pasipoti;

(c) nakala ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi au Kitambulisho cha Taifa cha wana kikundi au jumuiya; na

(d) taarifa ya shughuli husika zinazofanywa na kikundi au jumuiya.

(3) Kikundi au jumuiya ambayo itaomba usajili wa wanachama wake kikiwa hakina usajili au utambulisho wa kisheria kitawasilisha:

(a) hati yenye orodha halisi wana kikundi au jumuiya na utambulisho wao; na

(b) taarifa ya shughuli husika zinazofanywa na kikundi.

Mazingatio ya maombi.

12.-(1) Mkurugenzi Mwendeshaji, baada ya kupokea maombi ya usajili ya muombaji yaliyokamilika, atamsajili muombaji kuwa mwanachama katika Skimu na kumpatia kitambulisho cha uanachama.

(2) Endapo Mkurugenzi Mwendeshaji atakataa kumsajili muombaji chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, atamjulisha muombaji kwa maandishi na pamoja na sababu za kukataa huko.

(3) Mwanachama anaweza, endapo kitambulisho cha uanachama kilichotolewa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) kanuni hii kitapotea au kitaharibika, kuomba kupatiwa kitambulisho chengine, baada ya kupeleka taarifa kituo cha polisi na kupewa uthibitisho wa kupotea kitambulisho hicho.

(4) Mkurugenzi Mwendeshaji baada ya kupokea uthibitisho wa kupotea kwa kitambulisho chini ya kanuni ndogo ya (3) ya kanuni hii, atampatia muombaji kitambulisho chengine cha uanachama.

SEHEMU YA TANO
MICHANGO NA TARATIBU ZA UWASILISHAJI WA MICHANGO

Wajibu wa kuchangia katika Skimu.

13.-(1) Kila mwanachama wa Skimu ana wajibu wa kuchangia katika Skimu kiwango cha mchango kama ilivyoelezwa katika Sheria.

(2) Bodi inaweza kutoa muongozo juu ya viwango vya michango na masharti mengine ya uchangiaji kwa kadri itakavyoona inafaa.

Utaratibu na njia za kuwasilisha michango.

14. Michango chini ya Kanuni hizi itawasilishwa:

(a) katika hesabu maalumu za benki za Skimu;

(b) kwa njia ya fedha taslimu au hundi; au

(c) kwa njia ya uhaulishaji au amri ya malipo kutoka kwa wanachama; au

(d) njia nyengine yoyote ambayo Mkurugenzi Mwendeshaji ataona inafaa.

Uwasilishaji wa michango kwa wanachama wa kikundi.

15.-(1) Endapo kutakuwa na wanachama wa Skimu waliojiunga kama kikundi au jumuiya, kiongozi wa kikundi atawasilisha michango ya wanachama hao katika Skimu kwa mujibu wa utaratibu wa uwasilishaji michango uliowekwa katika Kanuni hizi.

(2) Michango itakayowasilishwa na kiongozi wa kikundi au jumuiya chini ya masharti kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, itawekwa katika hesabu ya kila mwanachama wa Skimu kutoka katika kikundi husika.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, mwanachama aliyejiunga kama kikundi au jumuiya anaweza kuongeza michango yake kwa kuchangia yeye mwenyewe binafsi wakati wowote atakapokuwa na uwezo wa kufanya hivyo baada ya kuwasilisha taarifa kwa maandishi ya kuonesha nia ya kuchangia mwenyewe na kukubaliwa na Mkurugenzi Mwendeshaji.

Mikataba ya upokeaji wa michango.

16. Skimu itatumia mikataba ifuatayo katika kupokea michango ya wanachama:

(a) mkataba wa ushirika au ubia;

(b) mkataba wa uwakala au uwezeshaji;

(c) mkataba wa mkopo usio na riba;

(d) mkataba wa mchango wa kujitolea; au

(e) mkataba mwengine wowote Bodi utakaoona unafaa.

Utoaji wa taarifa za Hesabu za mwana-chama.

17.-(1) Skimu itampatia mwanachama taarifa za mwenendo wa hesabu za michango yake pale mwanachama atakapozihitaji.

(2) Taarifa za hesabu za michango ya mwanachama zitatolewa kwa mwanachama mwenyewe, mwajiri au kwa kupitia kiongozi wa kikundi au jumuiya iwapo mwanachama huyo amesajiliwa au anachangia kupitia kikundi au jumuiya.

(3) Taarifa za mwanachama zitatolewa kwa taasisi husika za kiserikali pale itakapoonekana kuwepo haja ya kufanya hivyo na baada ya kupata idhini ya Mkurugenzi Mwendeshaji.

(4) Taarifa za mwenendo wa hesabu za michango ya mwanachama zinaweza kutolewa kwa njia ya tovuti, barua pepe, ujumbe wa simu ya mkononi, maandishi na njia nyengine zitakazoonekana zinafaa.

SEHEMU YA SITA
MAFAO, SIFA NA UTARATIBU WA MALIPO WA MAFAO

Mafao yataka-yolipwa na Skimu.

18.-(1) Skimu italipa mafao yafuatayo:

(a) fao la uzeeni;

(b) fao la ulemavu;

(c) fao la urithi;

(d) fao la uzazi;

(e) fao la upotevu wa ajira;

(f) fao la kuumia kazini; au

(g) fao jengine lolote kama Bodi itakavyoona inafaa.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Skimu haitaanzisha fao lolote jipya bila ya kuzingatia uwezo na uhimilivu wa Skimu katika kulipa fao hilo.

Sifa za kulipwa fao la uzeeni.

19. Mwanachama atalipwa fao la uzeeni kutoka katika Skimu endapo:

(a) amechangia katika Skimu kwa kipindi kisichopungua miezi miamoja na hamsini na sita; na

(b) amestaafu kazi kwa kutimiza umri wa lazima au umri wa hiari wa kustaafu.

Sifa za kulipwa fao la ulemavu.

20. Mwanachama atalipwa fao la ulemavu kutoka katika Skimu endapo:

(a) amechangia katika Skimu kwa kipindi kisichopungua miezi mia moja na hamsini na sita;

(b) amepata maradhi au ulemavu wa kudumu ambao umesababisha kutoweza kuendelea na kazi au kustaafishwa kazi.

Sifa za kulipwa fao la urithi.

21. Wategemezi wa mwanachama watalipwa fao la urithi kutoka katika Skimu iwapo mwanachama amefariki akiwa hajapokea mafao yake kutoka katika Skimu kwa mujibu wa utaratibu ulioelezwa katika Sheria na miongozo inayotolewa na Bodi.

Sifa za kulipwa fao la uzazi.

22. Mwanachama atalipwa fao la uzazi baada ya kutimiza sifa zilizoainishwa katika Sheria na miongozo.

Sifa za kulipwa fao la upotevu wa ajira.

23. Mwanachama atalipwa fao la upotevu wa ajira baada ya kutimiza sifa zilizoainishwa katika Sheria na miongozo.

Sifa za kulipwa fao la kuumia kazini.

24. Mwanachama atalipwa fao la kuumia kazini baada ya kutimiza sifa zilizoainishwa katika Sheria na miongozo.

Ukokotoaji wa mafao.

25. Mafao yanayolipwa na Skimu chini ya Kanuni hizi yatakokotolewa kwa mujibu wa viwango na utaratibu kama ilivyoelezwa katika miongozo.

Utaratibu wa kuomba mafao.

26.-(1) Mwanachama yeyote wa Skimu ataomba mafao yoyote anayostahiki kwa kujaza fomu maalumu na ataambatanisha na hati maalumu za kuthibitisha maombi ya mafao husika zilizoainishwa katika Muongozo wa Mafao uliotolewa na Bodi na atawasilisha fomu hizo kwa Mkurugenzi Mwendeshaji.

(2) Skimu itampatia mwanachama anayehusika na mafao au malipo yanayostahiki ndani ya siku kumi na nne za kazi baada ya mwanachama kukamilisha taratibu za maombi na Mkurugenzi Mwendeshaji kujiridhisha kuwa mwanachama huyo ana haki ya mafao anayoomba.

Kutostahili kupata mafao zaidi ya moja kwa wakati mmoja.

27. Endapo itatokea mwanachama wa Skimu ana sifa ya kulipwa mafao zaidi ya moja kwa wakati mmoja mwanachama huyo atalipwa fao moja tu ambalo litakuwa la kiwango kikubwa kuliko jengine.

SEHEMU YA SABA
UWEKEZAJI WA SKIMU

Taratibu za uwekezaji.

28.-(1) Skimu itawekeza fedha katika miradi salama na yenye tija kwa kufuata taratibu za tathmini ya uwekezaji salama zilizoidhinishwa na Bodi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya (1) ya kanuni hii, Skimu itahakikisha inazingatia Sharia au misingi ya Sharia katika kila aina ya uwekezaji itakayofanya.

Maeneo ya uwekezaji.

29. Skimu itawekeza katika maeneo yafuatayo:

(a) dhamana za serikali;

(b) hisa;

(c) amana ya uwekezaji wa muda maalumu;

(d) miradi ya majengo;

(e) hati ya uwekezaji;

(f) uwezeshaji; na

(g) maeneo mengine yatakayoidhinishwa na Bodi.

Mikataba itakayo-tumiwa na Skimu katika uwekezaji.

30. Skimu itafanya uwekezaji kwa kutumia mikataba ifuatayo:

(a) mkataba ya kuuziana;

(b) mkataba ya ushirika au ubia;

(c) mkataba ya ukodishaji;

(d) mkataba ya uwakala wa uwekezaji; na

(e) mkataba mwengine utakayothibitishwa na Kamati na kuidhinishwa na Bodi.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI YA FEDHA

Matumizi ya Fedha za Skimu.

31.Fedha za Skimu zitatumika kulipa mafao, kufanya uwekezaji na matumizi mengine yoyote ambayo Skimu itaona inafaa.

Hesabu za Skimu.

32. Skimu itaweka kumbukumbu na vitabu vya hesabu vya kila mwaka wa fedha vitakavyoonesha taarifa za mapato na matumizi ya Skimu pamoja na mali na madeni ya Skimu.

Bajeti ya Skimu.

33. Mkurugenzi Mwendeshaji katika kipindi cha miezi tatu kabla ya kumalizika mwaka wa fedha au katika kipindi chengine chochote kama itakavyoelekezwa na Bodi, atawasilisha kwa Bodi bajeti itakayoonesha makadirio ya mapato na matumizi ya Skimu kwa ajili kuidhinishwa na Bodi.

Ripoti za mwaka za Skimu.

34. Skimu, ndani ya kipindi cha miezi sita, baada ya kila mwisho wa mwaka, itawasilisha kwa Bodi ripoti ya mwaka itakayoonesha shughuli za Skimu kwa mwaka huo wa fedha.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI MENGINEYO

Michango kuwa katika dhamana ya Skimu.

35.-(1) Fedha na michango yote ambayo itakuwa katika hesabu za mwanachama, hadi itakapolipwa kwa mwanachama kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi, itakuwa kwenye dhamana ya Skimu na haitotumika kulipa madeni au madai yoyote yanayohusiana na mwanachama hata kama itakuwa kwa amri ya mwanachama.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, michango ya mwanachama inaweza kutumika kama dhamana kwa ajili ya uwezeshaji unaofuata misingi ya Sharia kutoka benki au taasisi za fedha zinazotoa uwezeshaji kwa kuzingatia misingi ya Sharia.

Tathmini ya uhimilivu wa Skimu.

36. Bodi itahakikisha kuwa Skimu inafanyiwa tathmini ya uhimilivu kila baada ya kipindi cha miaka mitatu au katika kipindi chengine chochote ambacho Bodi itaona kuwa inafaa ili kupima uhimilivu wa Skimu kutekeleza majukumu yake pamoja na rasilimali na madeni.

Makubaliano mbadala.

37. -(1) Skimu inaweza kufanya makubaliano mbadala na waajiri au taasisi mbalimbali kwa lengo la:

(a) mwajiri au taasisi kukata na kuwasilisha michango ya wanachama wa Skimu ambao ni wafanyakazi wake kwa masharti watakayokubaliana;

(b) kuwa na wakala wa ukusanyaji michango ya wanachama katika kikundi taasisi, nchi za kigeni ambapo kutakuwa na wanachama au mahali pengine popote.

JADWELI LA KWANZA

MAOMBI YA USAJILI WA MWANACHAMA
[Chini ya kanuni ya 10(1)]

SKIMU YA SHARIA ZSSF
SLP 2716
KILIMANI MNARA WA MBAO
ZANZIBAR

ISS - 1

KWA MATUMIZI YA OFISI TU	
ISS NAM:	
TAREHE YA	
KUJIUNGA	
SAINI	

FOMU YA KUJIUNGA

A. SEHEMU HII IJAZWE NA MWANACHAMA

1. Jina la mwajiri .....
2. Jina la Mwanachama: .....
3. Jinsia: M/me ☐ M/ke Tarehe ya kuzaliwa ☐
4. Anuani ya Kudumu: .....
5. Barua pepe: ..... Na. ya Simu.: .....
6. Aina ya kitambulisho: ..... Na. ya Kitambulisho.: .....
7. Tarehe ya kuanza kuchangia: .....
8. Aina ya uchangiaji: Mfuko Mkuu ☐ Uchangiaji wa hiari ☐
9. Jina la mama: .....
10. Jina la mume/mke wa mwanachama: .....
11. Jina la watoto wa mwanachama:
    (a) .....
    (b) .....
    (c) .....
    (d) .....
    (e) .....
12. SAINI YA MWANACHAMA PICHA YA MWANACHAMA

JADWELI LA PILI

FOMU YA MAOMBI YA USAJILI WA KIKUNDI AU JUMUIYA
[Chini ya kanuni ya 14(1)]

Nambari ya usajili | | | | | | |

ZSSF SHARIA SKIMU
S.L.P 2716
KILIMANI MNARA WA MBAO
ZANZIBAR

ISS - 4

KWA MATUMIZI YA OFISI TU	
ISS Nam:	
ENTRY DATE	
INITIALS	

Jina la kikundi/Jumuiya: _____

Idadi ya Wanachama: _____

Aina ya Biashara: _____

Anuani: _____

Mkoa: _____ Wilaya: _____

Mtaa: _____ Nam. ya Nyumba: _____

Sanduku la Posta: _____ Nukush: _____

Nambari ya Simu: _____ Barua pepe: _____

Tovuti: _____

SEHEMU B

Wasiliana: _____

Jina: _____

Cheo: _____ Nambari ya simu: _____

Barua pepe: _____

SEHEMU C

Taarifa za wanachama (Ikibidi tumia karatasi ya ziada)

S/No.	Jina la mwanachama	Nambari ya usajili
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		

Uthibitisho (Declaration)

Mimi..... **nathibitisha kuwa haya niliyoyaandika hapa kwa ufahamu wangu, ni kamili na ya kweli.**

ZIMETIWA saini tarehe 5 Mwezi Septemba 2025.

(DKT. SAADA MKUYA SALUM)
WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO
ZANZIBAR

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR-2025